



## TANGAZO LA MAENEO YA KUPANGISHA KWA AJILI YA KUTOLEA HUDUMA KWA WANAFUNZI WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kinapenda kuutangazia umma kuwa kimetenga eneo maalumu kwa ajili ya kutoa huduma kwa wanafunzi kama ifuatavyo:

NA.	ENEO	KAMPASI/MAHALI	HUDUMA INAYOTAKIWA
1.	Chumba kilichopo Jengo la Biashara la Dkt. J. P. J. Magufuli	Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere Mlimani	Supermarket

Kwa tangazo hili, UDSM inawaalika wale wote wenye nia na wanaopenda kutoa huduma hiyo kama ilivyoainishwa katika jedwali hapo juu kuomba kutoa huduma hiyo. Waombaji wafike Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliyopo Ofisi Namba 228 Jengo la Utawala (Cranford Pratt Building) kwa ajili ya kuchukua fomu za maombi. Waombaji watalipa shilingi elfu kumi tu (TZS 10,000/=) kupitia 'Namba ya Kumbukumbu' ambayo inapatikana Ofisi Namba 225 kwa Mhasibu wa Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji.

Mwisho wa kuchukua na kurudisha fomu ni siku kumi na nne (14) kutoka siku ya kwanza ya tangazo hili.

Tarehe **13 Desemba 2024** itakuwa ni siku ya kutembelea eneo lililotengwa kwa ajili ya kutolea huduma hiyo ambapo saa 4:00 asubuhi waombaji wote wanatakiwa kuwepo katika eneo la Jengo la Biashara la Dkt. J. P. J. Magufuli lililoko karibu na mabweni ya Dkt. J. P. J. Magufuli Kampasi ya Mwl. J. K. Nyerere Mlimani.

Baada ya mchakato wa kupata watoa huduma kukamilika, waombaji wote wataarifiwa juu ya matokeo ya maombi yao kwa njia ya barua.

**IMETOLEWA NA**  
**NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO – MIPANGO, FEDHA NA UTAWALA**  
**4.12.2024**